**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**
**Tovuti: www.hlpc.go.tz**
**Simu: 0734005777 Barua Pepe:hlpc@afya**

# TANGAZO

## MAOMBI YA MITIHANI YA USAJILI

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inapenda kuwataarifu wahitimu wote wa taalauma ya Maabara ambao wameshatumikia usajili wao wa awali kwa kipindi cha miezi 12 au zaidi, kuwa dirisha la maombi ya mitihani ya usajili kwa mwezi Oktoba 2024 litafunguliwa tarehe 15.08.2024 na kufungwa tarehe 15.09.2024 kwa ngazi zote.

Waombaji wate wanatakiwa kuhakikisha wanafanya maombi yao kupitia akaunti zao za mfumo wa hprs.moh.go.tz. Aidha wanakumbushwa kulipia ada ya mitihani kwa wakati kabla ya dirisha kufungwa.

Waombaji wote waliopata usajili wa awali nje mfumo wa hprs.moh.go.tz (Kabla ya Oktoba 2021) wanatakiwa watume taarifa zao Ofisi ya Msajili Baraza la Mataalam wa Maabara kabla ya Tarehe 15.08.2024 kupitia namba ya simu 0734005777). Taarifa za kutuma ni

- Jina kamili
- Barua pepe
- Namba ya simu
- Namba ya usajili wa awali
- Ngazi ya elimu ya Taaluma

**Aidha, waombaji wote wanatakiwa kuzingatia muda uliopangwa kwani taarifa au maombi yatakayowasilishwa baada ya muda uliopangwa hapo juu kupita hayatafanyiwa kazi.**

Nawatakiwa waombaji wote utekelezaji mwema.

Kwa msaada zaidi wasiliana na ofisi ya msajili

Imetolewa na:
Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
06.08.2024

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
06 AUG 2024
P.O.Box 743
DODOMA